
Ijue Biblia Yako

# I B A D A
# (WORSHIP)

**Mafunzo ya Biblia Ngazi ya Juu**



J e r r y  B a t e s

Ibada : Toleo la II, 2021

Mpangilio  na Tafsiri
(Layout and Translation)

**S h a d r a c k   S.  M s a m b a z a**

Uhariri
(Proof reading)

**P e t e r   K a m a t u l a**

Nakala kwa lugha ya Kiswahili na,

**SWAHILI GOSPEL TEAM (SGT)**
swahiligospelteam@gmail.com
Arusha, Tanzania

# YALIYOMO

1. Ibada ni Nini? 1

2. Ni wapi itupasapo kuabudia? 9

3. Sala 17

4. Meza ya Bwana 27

5. Uimbaji 35

6. Changizo ya Watakatifu (Utoaji) 45

## Utangulizi

Mwandishi wa kitabu hiki Bw. Jerry Bates, ni mhubiri na mwalimu mwenye uzoefu wa muda mrefu katika masomo ya Biblia. Pia amebobea katika uchambuzi na uandishi wa vitabu, ameandika vitabu mbalimbali vya kidini. Kama ilivyo katika vitabu vingine, katika kitabu hiki ameonesha umahiri wake wa ufundishaji kwa njia ya uandishi na kuhakikisha kila anayebahatika kusoma kitabu hiki anaelewa vizuri kuhusu ujumbe ambao Biblia inamzawadia kila mtu kwa upendo wa dhati utokao kwa Mungu wetu.

Kitabu hiki kinafafanua kwa undani kuhusu Ibada na matakwa ya Mungu katika namna impendezayo yenye matokeo ya Ibada ya roho na kweli (Yohana 4:24).

Kila mwisho wa mada kuna kipengele cha maswali ambacho ni mahususi kwa wewe kujipima katika kile ulichojifunza.

Tunapendekeza kitabu hiki kisomwe na kila mtu kama sehemu ya kujifunza Maandiko Matakatifu na kupata fursa ya kutenda kwa usahihi mapenzi ya Mungu. Tunakushukuru kwa kutenga muda wako ili usome kitabu hiki! Ni matumaini yetu utawashirikisha na wengine ujumbe utakaojifunza katika kitabu hiki.

“Amani na upendo wa Bwana wetu Yesu Kristo, katika ushirika wa Mungu Baba na Roho Mtakatifu uwe nawe daima!”

**Swahili Gospel Team (SGT)**
swahiligospelteam@gmail.com
**Arusha, Tanzania**

# 1

## IBADA NI NINI?

Moja kati ya shughuli muhimu ambazo Wakristo hujihusisha nazo ni tendo la ibada. Matendo mengi ambayo yameongezwa na watu katika ibada ya kisasa hayatoki katika mamlaka ya Neno la Mungu; hata hivyo, Paulo ameandika katika Wakolosai 3:17, **Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye.** Kufanya jambo fulani katika jina la Yesu ni kufanya katika mamlaka yake. Ibada, ambayo haitokani na mamlaka ya Kibiblia ni bure au ni ibada tupu kulingana na Yesu (**Mathayo 15:9**). Hivyo, tunahitajika kuhakikisha kile ambacho kimehusishwa katika ibada ya Kibiblia ili tuwe na uhakika ya kwamba ibada yetu inakubalika kwa Mungu.

### Ibada ni Nini?

Ka waida neno Ibada linalotafsiriwa katika Agano Jipya kumaanisha kunyenyekea, kusujudu au kuonesha heshima ya juu, linaashiria heshima kuu, uchaji, au kicho. Aya bora kuhusiana na ibada ni **Yohana 4:23-24, Lakini saa inakuja, nayo sasa ipo, ambayo waabuduo halisi watamwabudu Baba katika roho na kweli. Kwa maana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu. Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli.**

Kwa kuwa Yesu anazungumzia waabuduo halisi, hiyo inadokeza uwepo wa waabuduo batili. Mlengwa wa ibada yetu ni Mungu Baba. Hii inaashiria ukaribu na upendo (Waefeso 1:3, Luka 11:2-4), hata hivyo, kamwe hatupaswi kusahau heshima na hofu ambayo inamstahili Mungu. Mambo mawili yanayohusishwa kwenye ibada ya kweli, **roho** na **kweli**. Ibada iliyojaa **roho** ni ibada ya dhati itokayo katika moyo, na kuabudu katika **kweli** ni kuabudu kama Mungu alivyoelekeza katika Neno lake. Yesu alisema, "neno lako ndilo kweli" (Yohana 17:17); hivyo, kuabudu katika **kweli** ni kuabudu kama ilivyoelekezwa katika Neno lake.

Ibada ni kitendo cha kumuadhimisha Mungu. Tunapaswa kukumbuka kuwa Mungu ndiye mlengwa wa ibada yetu. Mhubiri mmoja alifafanua ibada kama "kumtambua Mungu kuwa ni nani, kujitambua mwenyewe kuwa ni nani, na kuitikia ipasavyo" Hii ni fafanuzi rahisi na itakuwa ikitumika kama msingi kwa ajili ya uelewa wa ibada katika somo hili. Kipengele cha kwanza cha ibada ni kumtambua Mungu kuwa ni nani. Mungu ni Muumba wa wote mbingu na dunia na vyote vilivyomo (Mwanzo 1:1, Wakolosai 1:16). Yeye ni Mungu pekee wa Kweli (Kutoka 20:2-3). Yeye ni mnyoofu hasa, mtakatifu na wa haki (Marko 10:18). Isaya anakazia kipengele hiki cha Mungu pale alipomwita "Mtakatifu wa Israeli". Isaya anatumia neno "Mtakatifu" katika kumrejea Mungu mara 29 (kwa mfano, Isaya 1:4; 43:15). Hili ni fumbo kuu. Mtakatifu yu kati yetu. **Paza sauti, piga kelele, mwenyeji wa Sayuni; Maana Mtakatifu wa Israeli ni mkuu kati yako. (Isaya 12:6).**

Pili, tujue sisi ni akina nani. Paulo ananukuu Zaburi 14:1-3 na Zaburi 53:1-3 katika Warumi 3:10-12 kuweka muhtasari wa hatima ya mwanadamu. **Hakuna mwenye haki hata mmoja. Hakuna afahamuye; Hakuna amtafutaye Mungu. Wote wamepotoka, wameoza wote pia; Hakuna mtenda mema, la! Hata mmoja.** Hata baada ya kupita jaribu kuu la imani yake, Ayubu anasema, **Kwa sababu hiyo najichukia nafsi yangu, na kutubu Katika mavumbi na majivu. (Ayubu 42:6).** Pindi nabii mwaminifu Isaya alipopokea maono kutoka kwa Mungu, alikiri kwamba alikuwa ni **mtu mwenye midomo michafu (Isaya 6:5).** Hivyo, tunaona kwamba pale ambapo mara nyingi tunapojiona kama watu wazuri, ukalinganisha na Mungu, sisi ni viumbe watenda dhambi. Kiwango cha Mungu ni kamili, ambacho kwa kweli ni bora sana kuliko kiwango cha wema wa mwanadamu. Hivyo, katika ibada mtu utambua dhambi zake na asivyostahili kumkaribia Mungu (Luka 5:8; Isaya 6:5). Hii inakuza shukrani na unyenyekevu kwa upande wa mcha Mungu.

Tatu, tunapaswa kuitikia ipasavyo. Mwitikio upasao ni nini? Sababu mbalimbali zimehusishwa katika ipasavyo mwitikio wetu. (1) Tunapaswa kuwa na dhana ya namna utegemezi na unyenyekevu. Mungu ni muumbaji wa yote, sisi wote tumetoka kwake. (2) tunapaswa kuwa na tabia ya kushukuru. Biblia mara nyingi inasisitiza kushukuru kwa upande wa mwanadamu. **Na kumshukuru Mungu Baba siku zote kwa mambo yote, katika jina lake Bwana wetu Yesu Kristo;** (Waefeso 5:20). (3) Vile vile tunapaswa kujaa

furaha. **Furahini katika Bwana sikuzote; tena nasema, Furahini.**(Wafilipi 4:4). **Basi Mungu wa tumaini na awajaze ninyi furaha yote na amani katika kuamini, mpate kuzidi sana kuwa na tumaini, katika nguvu za Roho Mtakatifu.** (Warumi 15:13). (4) Ni lazima tusalimishe maisha yetu katika mapenzi yake kwa utiifu. **Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. (Warumi 12:1).** Haitoshi tu kuabudu kwa usahihi; ni lazima ibada itoe matokeo ya maisha ya utakatifu. Hatuwezi kuitenganisha ibada yetu na namna tunavyoishi maisha yetu. Ikiwa ibada yetu haiambatani na maisha ya utakatifu, Mungu ataichukia. **Mimi nazichukia sikukuu zenu, nazidharau, nami sitapendezwa na makutano yenu ya dini. Naam, ijapokuwa mnanitolea sadaka zenu za kuteketezwa na sadaka zenu za unga, sitazikubali; wala sitaziangalia sadaka zenu za amani, na za wanyama walionona.** (Amosi 5:21-22). Tatizo katika siku za Amosi haikuwa kwamba wana wa Israeli walikuwa wakiabudu isivyosahihi, bali ibada yao haikuleta matokeo ya maisha ya utakatifu, hivyo, Mungu akagoma kupokea ibada yao.

## Makusudio ya Ibada

Biblia inatuambia kuwa kuna makusuduo kadhaa ya ibada. Bila shaka, kusudio kuu ni kumpa Mungu utukufu. **Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lo lote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu.** (1 Wakorintho 10:31). Ni Mungu pekee anayestahili kutukuzwa na kupewa utukufu. Inatakiwa Mungu aonekane akiishi ndani yetu kupitia kila tendo tufanyalo, na hakuna njia bora ya kufanya hivi zaidi ya ibada. Katika waraka kwa Waefeso Paulo aliomba kwamba, **naam, atukuzwe katika Kanisa na katika Kristo Yesu hata vizazi vyote vya milele na milele. Amina.** (Waefeso 3:21). Kususdi la pili ni kuwajenga Wakristo**. wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane; na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia.** (Waebrania 10:25).kwa mara nyingine hii inasisitiza umuhimu wa kukusanyika, kwa sababu, ni wazi, bila ya kukusanyika pamoja kamwe hatuwezi kufarijiana. Paulo pia aliwaambia Wakorintho katika 1 Wakorintho 14:26 **Mambo yote na yatendeke kwa kusudi la kujenga.** Maneno “kuinua” au “kujenga” yametumika mara saba katika 1 Wakorintho 14. Paulo alikuwa anarekebisha matumizi mabaya ya ibada pamoja na karama za kiroho. Kwasababu kujenga[na] kunahitaji maelekezo na hotuba inayoeleweka. Hata hivyo, tunaona kwamba moja kati ya malengo makuu ni kuwajenga Wakristo. Kusudi lingine la ibada ni kuadhimisha au kutangaza wokovu wetu na umoja wetu kwa pamoja kama mwili wa Kristo. **Kikombe kile cha baraka tukibarikicho, je! Si ushirika wa damu ya Kristo?**

**Mkate ule tuumegao, si ushirika wa mwili wa Kristo? Kwa kuwa mkate ni mmoja, sisi tulio wengi tu mwili mmoja; kwa maana sisi sote twapokea sehemu ya ule mkate mmoja.** (1 Wakorintho 10:16-17). Katika sura inayofuata, wakati Paulo akirekebisha matumizi mabaya ya Meza ya Bwana, aliandika katika aya ya 26, **Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo.** Kwa hiyo, tunaposhiriki Meza ya Bwana, tunatangaza au kufundisha wale wasio Wakristo ambao huenda wamehudhuria ibada, juu ya dhabihu na kifo cha Yesu, hali kadhalika kuwakumbusha Wakristo wenzetu juu ya wokovu wetu mkuu na umoja tulionao kama washirika wa mwili wa Kristo.

## Hitimisho

Katika somo hili tumejifunza nini maana ya ibada na baadhi ya makusudio ya ibada. Matumizi mengi mabaya ya ibada za siku hizi yametokea kwa sababu tumesahau kusudi la ibada na kugeukia katika jambo la kujipendeza nafsi zetu. Katika masomo yajayo tutaangalia kwa undani kila kipengele kinachohusishwa katika ibada yetu kwa Mungu.

## Maswali ya kujipima

1. Sababu mbili za ibada ya kweli ni zipi?

2. Kuabudu katika roho kuna maanisha nini?

3. Kuabudu katika kweli kuna maanisha nini?

4. Sehemu tatu za ibada ya kweli ni zipi kulingana na fafanuzi iliyotumika katika somo hili?

5. Mungu ni ____________________ wa Israeli kulingana na Isaya.

Kweli / Si kweli

1. Ibada kimsingi ni lazima ielekezwe kwa Mungu. Kweli / Si kweli.

2. Ibada inaashiria kutoa heshima, kicho au uchaji. Kweli / Si kweli.

3. Ibada imetengana kabisa na maisha yetu yote, kwa hiyo, ibada ya mtu inaweza kukubalika ingawa anaishi maisha ya dhambi. Kweli / Si kweli.

4. Yote tufanyayo katika maisha yanapaswa kumpa Mungu heshima na utukufu. Kweli / Si kweli.

5. Kimsingi ibada ni baina ya Mungu na mtu Mmoja mmoja, kwa hiyo, tunawafikiria kidogo Wakristo wenzetu wanaotuzunguka. Kweli / Si kweli.

# 2

## NI WAPI ITUPASAPO KUABUDIA?

Wanaume na wanawake siku zote wamemsogelea Mungu katika ibada. Hata mwanzoni kabisa, tunaona Kaini na Habili wakileta sadaka kwa Mungu. (Mwanzo 4:15). Tunasoma ya kwamba pindi wote walipoleta sadaka kwa Mungu ni sadaka ya Habili pekee ndiyo iloyokubaliwa na Mungu. Katika kipindi cha mababa, kila familia ilitoa sadaka zao wenyewe kwa Mungu katika ibada. Wakati Mungu alipofanya Agano na wana wa Israeli katika Mlima Sinai, Mungu alibainisha kwamba ibada zote zifanyike katika Hema ya kukutania kwa kupitia makuhani wa kabila la Lawi. Baadaye, mchakato wa kuanzisha ufalme mwanzoni mwa mfalme Sauli, Hekalu la Yerusalemu lilichukua nafasi ya Hema. Hivyo, kuanzia hapo na kuendelea, ibada ilifanyika Yerusalemu. Hata hivyo, chini ya Agano lililoasisiwa na Kristo, ibada inaweza kufanyika popote. Wakati Yesu alipokuwa akizungumza na mwanamke msamaria kisimani katika Yohana 4, Yule mwanamke alimuuliza Yesu kuwa ni wapi mahala sahihi pa kuabudia. Mababa zake walisema kuwa Samaria ndiyo sehemu sahihi, Wayahudi nao walidai kuwa Yerusalemu ndipo sehemu sahihi. **Yesu akamwambia, Mama, unisadiki, saa inakuja ambayo hamtamwabudu Baba katika mlima huu, wala kule Yerusalemu.** (Yohana 4:21). Kwa maneno mengine, eneo tunapoabudia si muhimu. Sasa, watu wa Mungu wanapatikana katika kila taifa

ulimwenguni, hivyo wanaweza kumwabudu Mungu katika taifa lo lote walipo.

## Tunapaswa Kuabudu Lini?

Katika kipindi cha Sheria ya Musa, Israeli waliamriwa kuabudu katika siku ya Sabato. **Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote;… Maana, kwa siku sita Bwana alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo Bwana akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa.** (Kutoka 20:8-11). Agano hili walipewa waisraeli pekee. Baadaye, Musa aliandika**, Bwana, Mungu wetu, alifanya agano nasi katika Horebu.Bwana hakufanya agano hili na baba zetu, bali na sisi, yaani, sisi sote tuliopo hapa, tu hai.** (**Kumbukumbu La Torati 5:2-3**). Agano hili, ambalo lilijumuisha kuishika siku ya Sabato, lilifanyika kwa wana wa Israeli na vizazi vyao pekee wala si na baba zao wala watu wa mataifa. Yesu aliligongomelea agano hili katika msalaba wake. **akiisha kuifuta ile hati iliyoandikwa ya kutushitaki kwa hukumu zake, iliyokuwa na uadui kwetu; akaiondoa isiwepo tena, akaigongomea msalabani;** (Wakolosai 2:14). Katika Warumi 7, Paulo alifundisha kwamba tuliifia sheria ili tuwe mali ya mwingine (Kristo). Halafu katika aya ya 7, anabainisha kwa kutaja amri "usitamani" kama moja kati ya amri ambazo tumezifia. Hiyo ni moja kati ya amri kumi (Kutoka 20:17). Kama mtu ameifia amri moja kati ya Amri kumi, basi ni lazima amezifia zote. Hivyo, hatuamrishwi tena kuishika siku ya Sabato na kututaka kuabudu katika siku hiyo. Chini ya Agano Jipya, tunaona

kwamba tunatakiwa kuabudu katika siku ya kwanza ya juma. Kanisa la kwanza tangu mwanzo waliabudu katika siku ya kwanza ya juma. Paulo alikutana na Kanisa huko Troa katika siku ya kwanza ya juma (Mdo 20:7). Hata hivyo, alikaa pale katika mji kwa siku saba, jambo linaloashiria kwamba huu haukuwa mkutano maalum wa kumsikiliza Paulo, isipokuwa ni kawaida na utamaduni wa siku ya ibada. **Walikutana pamoja kumega makate** (kushiriki Meza ya Bwana), si kwamba kusikiliza mahubiri ya Paulo. Alikuwepo pale hata siku ya Sabato, lakini alikusanyika nao kuabudu katika siku ya kwanza ya juma. Paulo aliamuru kanisa la Korintho kutoa changizo katika siku ya kwanza ya juma (1 Wakorintho 16:2), ambayo kwa mara nyingine hii inaashiria kwamba ilikuwa ni desturi kuabudu katika siku hii. Ni jambo la kawaida kwa kanisa la kwanza kuabudu katika siku ya kwanza ya juma, sababu na umuhimu wa hayo yote ni kwamba ilitokana na uanzishwaji wa kanisa kutokea katika siku ya kwanza. Yesu alifufuka kutoka kwa wafu katika siku ya kwanza ya juma. Akina mama walikuja kaburini alfajiri mapema katika siku ya kwanza ya juma (Luka 24:1). Wakati wakiwa kaburini wanaume wawili waliovalia mavazi ya kung'aa (24:4) waliwakumbusha maneno ya Yesu, **aliyosema, Imempasa Mwana wa Adamu kutiwa mikononi mwa wenye dhambi, na kusulibiwa, na kufufuka siku ya tatu.** (24:7)**.** Kwa kuwa Yesu alisulibiwa Ijumaa, siku ya tatu ingekuwa Jumapili, kulingana na Wayahudi walivyokokotoa muda, wakihesabu kila kipande cha siku kama siku nzima. Siku hiyo hiyo, watu wawili walikuwa wakisafiri kuelekea katika kijiji kilichoitwa Emau (24:13), na Yesu akawatokea lakini hawakumtambua. Wakati

wakizungumza watu hawa walisema, **Nasi tulikuwa tukitumaini ya kuwa yeye ndiye atakayewakomboa Israeli. Zaidi ya hayo yote, leo ni siku ya tatu tangu yalipotendeka mambo hayo;** (24:21). Hivyo, tunaona kwamba Wakristo walijua kwamba Kristo alitabiri kufufuka katika siku ya kwanza ya juma. Yesu alikutana na wanafunzi wake katika siku ya kwanza ya juma (Yohana 20:19), lakini Tomaso hakuwepo katika tukio hilo. Katika siku ya kwanza iliyofuata (20:26), Yesu aliwatokea tena wanafunzi wake wakati huu Tomaso akiwepo. Kanisa lilianzishwa katika siku ya Pentekoste, ambayo wakati wote ilikuja katika siku ya kwanza ya juma (Mambo ya Walawi 23:15-16). Ilikuwa ni siku hii ambayo Roho Mtakatifu aliwashukia mitume, na hotuba ya kwanza ya injili ilihubiriwa kutimiza unabii wa Isaya 2:2-4. Siku hiyo hiyo, watu 3,000 walibatizwa, hivyo kanisa likaanzishwa (Mdo 2:41). Tangu hapo, tunasoma tu habari ya kanisa wakiabudu katika siku ya kwanza ya juma hata ingawa Wakristo wa awali wote walikuwa Wayahudi, ambao siku zote waliabudu katika siku ya Sabato.

## Kuhubiri au Kufundisha

Moja kati ya vipengele muhimu katika ibada yetu ni kujifunza neno la Mungu. Desturi, mtu mmoja anawakilisha hotuba au maonyo akiwa katika nafasi ya neno la Mungu, lakini hiyo si njia pekee ya kujifunza neno la Mungu kwa pamoja. Cha msingi ni kwamba neno la Mungu linafundishwa ili kanisa lijengwe. Vifungu vingi vinasisitiza kufundisha neno la Mungu. Paulo alihutubu katika kanisa huko Troa mpaka usiku wa

manane (Mdo 20:7). **Kwa sababu hii nimemtuma Timotheo kwenu, aliye mwanangu mpendwa, mwaminifu katika Bwana, atakayewakumbusha njia zangu zilizo katika Kristo, kama vile nifundishavyo kila mahali katika kila kanisa**. (1 Wakorintho 4:17). **Nakuagiza mbele za Mungu, na mbele za Kristo Yesu, atakayewahukumu walio hai na waliokufa; kwa kufunuliwa kwake na kwa ufalme wake; lihubiri neno, uwe tayari, wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho**. (2 Timotheo 4:1-2). Mungu alichagua mahubiri kama njia ya injili yake iokoayo. **Kwa maana katika hekima ya Mungu, dunia isipopata kumjua Mungu kwa hekima yake, Mungu alipenda kuwaokoa waaminio kwa upuzi wa lile neno linalohubiriwa.** (1 Wakorintho 1:21). Paulo alisema kwamba hakuazimu kujua neno lo lote kwa Wakorintho isipokuwa Yesu Kristo, aliyesulubiwa(1 Wakorintho 2:2), na hakuhubiri kwa maneno yenye kushawishi yenye hikima ya binadamu (1 Wakorintho 2:4). katika 1 Wakorintho 14 Paulo alikuwa akiandika kurekebisha matumizi mabaya ya karama za unabii na aina za lugha. Lengo la msingi lilikuwa ni kwamba kanisa lijengwe (14:4-5), kitu ambacho kingeweza kutokea kama watu wangeelewa kilichosemwa. Angalia hitimisho la Paulo katika aya ya 26, **mambo yote na yatendeke kwa kusudi la kujenga**. Kwa uelewa wa neno la Mungu tu, mtu anaweza kujengwa kiroho, kwa hiyo tunaweza kuona umuhimu wa kuhubiri au kufundisha neno la Mungu katika mkusanyiko wa ibada. Kuhubiri au kufundisha ni kipengele muhimu katika ibada. Kuhubiri si aina ya mtindo wa kuburudisha au muda wa mtu

kuonesha ujuzi wake wa kuzungumza. Kuhubiri humwezesha muumini kuona na kumsikia Mungu. Mwalimu anatakiwa kuleta ujumbe wa Mungu kwa wasikilizaji wake. Mahubiri yatamwezesha mtu kulifanyia kazi Neno katika maisha yake. Hali kadhalika mahubiri humwezesha mtu kumwona Mungu, kujikagua wenyewe, na kuona kazi yetu katika nuru ya neno la Mungu. Tunapaswa kukumbuka kwamba kuhubiri hakuna mpaka kwa mtu fulani kuwa na mafunzo maalumu ya kuhubiri. Elimu ya Biblia inahitajika na ina msaada mkubwa, [lakini] kila mtu anaweza kuhubiri, ikiwa ana uwezo, na shauku ya kujiandaa mwenyewe kwa utafiti wa kina, hapo anapaswa kuruhusiwa kuhubiri, hata kama amejifundisha mwenyewe. Mahubiri hayajawekewa mpaka kwa “viongozi”. Wazo hilo ni uvumbuzi wa binadamu wala Biblia haifundishi hivyo.

## Maswali ya kujipima

1. Ni siku ipi Wayahudi waliamriwa kuabudu?

2. Lini agano la kale liliondolewa?

3. Ni siku ipi Yesu alifufuka kutoka kwa wafu?

4. Ni siku ipi ambayo Yesu alikutana na wanafunzi wake baada kufufuka kwake na baina ya kupaa kwake?

5. Kusudi la msingi la mwalimu katika ibada yetu ni lipi?

Kweli / Si kweli

1. Katika kipindi cha mababa, kila kaya ilileta sadaka yao kwa Mungu na kutoa wenyewe. Kweli / Si kweli.

2. Kanisa la kwanza waliabudu siku ya Sabato kwa kuwa wengi wao walikuwa Wayahudi. Kweli / Si kweli.

3. Siku ya Pentekoste siku zote ilikwa ni siku ya kwanza ya juma. Kweli / Si kweli.

4. Kanuni ya msingi kukumbuka katika ibada yetu ni kwamba mambo yote yatendeke kwa kusudi la kujenga. Kweli / Si kweli.

5. Mahubiri yanatakiwa yafanywe na wale wenye mafunzo maalumu, kwa mfano viongozi. Kweli / Si kweli.

# 3

# SALA

Ni wazi sala ni kipengele muhimu katika ibada yetu kwa Mungu, na mara nyingi Biblia husisitiza umuhimu wake. Angalia aya hizi chache kwa ujumla kuhusu sala. **Akawaambia mfano, ya kwamba imewapasa kumwomba Mungu siku zote, wala wasikate tamaa.** (Luka 18:1). **kwa tumaini, mkifurahi; katika dhiki, mkisubiri; katika kusali, mkidumu**; (Warumi 12:12). **kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote;** (Waefeso 6:18).

## Sala ni nini?

Kwanza na zaidi sana, tunapaswa kukumbuka kwamba sala ni njia ya sisi kuzungumza na Mungu. Inatakiwa kumwelekea Mungu, kwa uaminifu mkubwa Kwake. Iwe ni kwa dhati au kutoka moyoni. Si tu kutamka maneno sahihi, kama vile dua za kichawi. Inapaswa kuwa ni tabia yetu. Paulo aliandika katika 1 Wathesalonike 5:17 kwamba tunapaswa kuomba bila ya kukoma. Kwa hakika, Paulo hasemi kwamba tunapaswa kuwa na maombi katika akili zetu na katika midomo yetu masaa 24 kwa siku. **Kuomba bila kukoma** kifupi inamaanisha kwamba Mungu hayuko mbali na mawazo yetu, na ya kwamba mioyo yetu, maisha yetu, na akili ziwe katika namna ambayo sala ni

sehemu ya maisha yetu ya kawaida. Kila wakati, tunaweza kuomba kimya kimya sala fupi tukimwomba Mungu atuongoze, atusaidie n.k.  kanisa la kwanza lilidumu katika maombi (Mdo 2:42).

Maombi si njia ya mazingaombwe au njia ya mkato kwa ajili ya mali na ubinafsi. Kwa kuwa Mungu ameahidi kusikia maombi ya watu wake (Mathato 21:22), tunapaswa kukumbuka kwamba mambo yote yako chini ya mapenzi yake. Katika Yakobo 4:1-6, Yakobo alizungumzia juu ya Wakristo ambao walimwomba Mungu vitu [fulani], lakini hawakupata habari. Yakobo aliweka bayana kuwa maombi yao hayakukubaliwa kwa sababu yalikuwa ni ya ubinafsi, wakitaka vitu hivyo kwa ajili ya anasa zao. Hivyo, hatupaswi kuchukulia maombi kama vile hundi tupu ya malipo kutoka kwa Mungu, tunachohitajika kufanya ni kuomba na kusubiri kupokea.

Maombi si sharti. Sharti ni pale ambapo tunajaribu kupatana na Mungu kama vile kusema, “Kama utanibariki, nitaanza kukutumikia.” Mungu anastahili utumishi wetu kulingana na kile alichotutendea tayari, na kwa namna yo yote hatuwezi kumlazimisha Mungu kutubariki zaidi kwa ahadi zetu tupu za huduma. Wala hatupaswi kuchukulia maombi kama jambo fulani linalofaa wakati wa dharula tu. Wakati wa shida, wengi humgeukia Mungu kwa maombi. Lakini shida zikipita, wanamsahau Mungu na kuendelea na maisha yao kama hapo awali.

## Nani anayepaswa kuomba?

Watu wengi wangeweza kujibu hilo kwa haraka wakisema kila mtu anapswa kuomba, na kwa hakika nisingependa kumvunja moyo yeyote kwa habari ya kuomba. Tunapaswa kuelewa ya kwamba maombi ni matokeo ya baraka iliyohifadhiwa kwa ajili ya watoto wa Mungu. Wale ambao hawako katika famila ya Mungu hawana ahadi ya kwamba Mungu atasikiliza maombi yao. **Bwana yu mbali na wasio haki; Bali huisikia sala ya mwenye haki.** (Mithali 15:29). Katika 1 Petro 3:12, Petro ananukuu kutoka Zaburi 34 maneno haya, **Macho ya Bwana huwaelekea wenye haki, Na masikio yake hukielekea kilio chao Uso wa Bwana ni juu ya watenda mabaya, Aliondoe kumbukumbu lao duniani.** Aya nyingine zingeweza kuongezwa katika hizo, lakini kumbuka ya kwamba aya zote ambazo zinazungumzia sala wameandikiwa watu wa Mungu au Wakristo. Zaidi ya hivyo, ni wale Wakristo tu wanaoishi maisha ya haki ndio wenye fursa ya sala. Yohana aliandika katika 1 Yohana 3:22, **na lo lote tuombalo, twalipokea kwake, kwa kuwa twazishika amri zake, na kuyatenda yapendezayo machoni pake.** Tazama, Yohana anaandika kwamba wale ambao wanashika amri za Mungu wameahidiwa kwamba Mungu atajibu maombi yao. Hii inamaanisha kwamba wale wanaoishi maisha ya ukaidi hawawezi kufurahia ahadi hiyo. Wakristo wameamriwa kuombeana. **Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii.** (Yakobo 5:16). Maneno hayo wameandikiwa Wakristo wote, na tunaambiwa kwamba

maombi ya mwenye haki yana nguvu sana, sio tu yale ya mhubiri au mchungaji. Hakuna sehemu yeyote tuliyoamriwa tukaungame kwa padre, wala kamwe haikumaanisha kuwa maombi ya mhubiri au padre [mchungaji] kwa kiasi fulani yana nguvu zaidi au yana ufanisi zaidi kuliko maombi ya mtu mwingine yeyote. Kilicho muhimu ni maisha ya mtu, na siyo cheo alicho nacho. Halikadhalika maombi siyo mbadala wa utiifu. Kuna nyakati chache ambapo Mungu kwa hakika alimwambia mtu fulani kuacha kuomba (kwa mfano., Kutoka 14:15; Mdo 22:16). katika 1 Timotheo 2:8 Paulo anaandika, **Basi, nataka wanaume wasalishe kila mahali, huku wakiinua mikono iliyotakata pasipo hasira wala majadiliano.** Neno la Kiyunani wanaume katika kifungu hiki kinarejelea wanaume pekee. Kuna maneno mengine hutumika kwa wanawake au binadamu kwa ujumla. Hivyo, Paulo anaweka zuio kuwa maombi ya jumuiya yaongozwe na wanaume. Mara nyingi watu huuliza kuhusu kunyanyua mikono katika sala. Hakuna ubaya kuomba huku mikono imenyanyuliwa, [swala ni kwamba] hilo halikuamriwa. Katika Maandiko [kuna] watu wametajwa wakiomba katika mikao mbalimbali, lakini mara nyingi zaidi wametajwa wakiwa wanapiga magoti au kulala kifudifudi. Mikao ya kimwili si muhimu katika sala, bali, Paulo anasisitiza utakatifu wa maisha yetu. Wanaume waombaji ni lazima wawe watakatifu, wakiishi maisha ya utiifu.

## Tunapaswa Kuomba kwa ajili gani?

Mambo mengi yanatakiwa kujumuishwa katika maombi. La msingi zaidi, tunampa Mungu sifa. Mungu pekee ndiye anayestahili kutukuzwa. Sambamba na hili tunatoa shukurani zetu kwa ajili ya baraka zake zote za kimwili na zaidi sana za kiroho**. Msijisumbue kwa neno lo lote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu.**

**Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu. (Wafilipi 4"6,7). Dumuni sana katika kuomba, mkikesha katika kuomba huku na shukrani;** (Wakolosai 4:2). Tazama kwamba Paulo pia anajumuisha mahitaji binafsi katika sala zetu. Si ubinafsi au dhambi kumuomba Mungu kwa ajili ya baraka binafsi. Tunatakiwa pia kumwomba Mungu kwa ajili ya mwongozo (Yakobo 1:5). Tunapaswa kuwaombea wengine, kama vile, mafukara, wagonjwa, wafalme Wakristo wengine n.k (Yakobo 5:16). Sehemu ya msingi hasa ya maombi yetu ni kuungama, kukiri imani yetu na dhambi zetu. 1 Yohana 1:8 inasema kwamba tukiziungama dhambi zetu, Mungu ni mwaminifu atatusamehe. Ni wazi, ukiri huunganishwa na toba na hitaji la msamaha. Mungu ni mwaminifu, wakutegemewa, au wa kuaminika. Mungu ameahidi kutusamehe, na tunaweza kumwamini Mungu kwa kutenda kile alichoahidi. Hata hivyo, tunatakiwa kukumbuka kwamba tusipowasamehe wengine Mungu hatatusamehe na sisi (Marko 11:26).

## Tunapaswa Kuomba kwa jinsi gani?

Sehemu ya msingi zaidi katika maombi yetu ni dhamira yetu. Maombi yetu ni lazima yatokane na nguvu ya imani katika Mungu na moyo wa kweli. **Watu hawa huniheshimu kwa midomo; Ila mioyo yao iko mbali nami.** (Mathayo 15:8). Kinachojumuishwa katika moyo wa dhati ni unyenyekevu na kuomba kwa dhamira njema. Si lazima kuwa na sala ndefu. Katika Mathayo 6:5-8 Yesu aliwalaumu mataifa kwa kupayuka. Kwa kutamka mambo hayo hayo tena na tena hakufanyi maombi yetu kuwa na ufanisi. Maombi yaliyowekwa kumbukumbu ya watu mashuhuri wa imani yako kwa kifupi sana. Tunapaswa kumwomba Mungu kwa heshima. Ni lazima tukumbuke kwamba Mungu ni Mungu na sisi ni wanadamu tu.

**Usiseme maneno ya ujinga kwa kinywa chako, wala moyo wako usiwe na haraka kunena mbele za Mungu; kwa maana, Mungu yuko mbinguni, na wewe upo chini, Kwa hiyo maneno yako na yawe machache.** (Mhubiri 5:2). Tunatakiwa kumwomba Mungu katika jina la Yesu kama Mpatanishi wetu. Paulo aliandika, **Kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu;** (1 Timotheo 2:5). Mpatanishi ni yule anayesimama baina ya pande mbili, kwa jambo hili, pande mbili ni Mungu na binadamu, mpatanishi mzuri ni yule anayejua mazingira ya pande zote mbili, hivyo, hakuna aliye mpatanishi bora kama Yesu. Yeye anamjua Mungu, kwa sababu Yeye ni Mungu [pia], anawajua wanadamu, kwa sababu

alifanyika mwili kama binadamu (Wafilipi 2:5-11). Paulo pia alituhakikishia kwamba Roho Mtakatifu ana sehemu katika uwakilishaji wa maombi yetu kwa Mungu, **Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo, lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa. Na yeye aichunguzaye mioyo aijua nia ya Roho ilivyo, kwa kuwa huwaombea watakatifu kama apendavyo Mungu.** (Warumi 8:26-27). Huku kuugua si namna fulani ya lugha ya kiroho ijulikanayo na Mungu tu, ila ni kuugua kwa Roho, na sio mwanadamu. Ingawa tunaweza tukawa hatuelewi mambo yote ambayo Roho hutenda, tunaweza kuwa na uhakika ya kwamba Roho na Kristo huchukua maombi yetu na kuyawasilisha mbele za Mungu kulingana na mapenzi yake. Hili linapaswa kuwa faraja kubwa kwetu.

Sala pia inadokeza kuwa tutafanya kile tuwezacho kujibu maombi yetu. Maombi si njia rahisi ya kuwasaidia wengine bila kufanya chochote. Yakobo alionya dhidi ya tabia hii katika Yakobo 2:15-16; **Ikiwa ndugu mwanamume au ndugu mwanamke yu uchi na kupungukiwa na riziki, na mtu wa kwenu akawaambia, Enendeni zenu kwa amani, mkaote moto na kushiba, lakini asiwape mahitaji ya mwili, yafaa nini?** Kwa maneno mengine, haileti maana kama tukimwombea tu mtu, ni lazima tuwasaidie wale wenye mahitaji. Mungu anajibu maombi kwa kupitia watumishi wake, kwa hiyo, hatuwezi kumwombea tu mtu wakati kwa hakika hatufanyi jambo lo lote na kudhani kuwa tumetimiza wajibu wetu.

## Maswali ya kujipima

1. Sala ni nini?

2. Kuomba bila kukoma maana yake nini?

3. Tunapaswa kuungama dhambi zetu kwa nini?

4. Ni mambo gani ambayo yanapaswa kujumuishwa katika maombi yetu?

5. Ni kwa jinsi gani Roho utuombea?

Kweli / Si kweli

1. Maombi ni baraka iliyohifadhiwa kwa ajili ya wana wa Mungu pekee. Kweli / Si kweli.

2. Maombi ya mhubiri au padre [mchungaji] yana nguvu na maana sana. Kweli / Si kweli.

3. Katika ulimwengu wa leo, mtu yeyote anapaswa kuwa na uwezo wa kuongoza sala katika jumuiya. Kweli / Si kweli.

4. Maombi yetu yanapaswa kuombwa katika jina la Yesu ambaye ni mpatanishi. Kweli / Si kweli.

5. Kufanya jitihada yoyote binafsi ya kuwasaidia mafukara baada ya kuwaombea inaonesha ukosefu wa imani kwa Mungu na nguvu ya maombi. Kweli / Si kweli.

4

# MEZA YA BWANA

Kwa Mkristo yeyote, Meza ya Bwana, ambayo pia inaweza kuitwa ushirika, inapaswa kuwa sehemu muhimu katika ibada yetu. Maeneo makuu ya maandiko ambayo yanatuelekeza kuhusiana na Meza ya Bwana ni Mathayo 26:26-29; Luka 22:14-20 na 1 Wakorintho 11:23-34. Kuna mawazo kadhaa ambayo yanahusiana na Meza ya Bwana. (1) Ni kutoa shukurani. Wakati Yesu alipoanzisha Meza ya Bwana alishukuru. Tunapaswa pia kuwa na shukurani kwa dhabihu kuu ya Kristo kwa ajili yetu. (2) Ni kumbukumbu. Kumbukumbu inarudisha nyuma akili zetu katika baadhi ya mambo yaliyopita, na ushirika [Meza ya Bwana] inapeleka akili zetu nyuma katika msalaba wa Yesu. Katika 1 Wakorintho 11:25, tunaambiwa tushiriki ili kumkumbuka Yesu. (3) Tunaonesha au kutangaza mauti ya Bwana. **Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo.** (1 Wakorintho 11:26). Hivyo, Meza ya Bwana kwa upande fulani ni njia ya Kuhubiri, tunatangaza kwa matendo yetu imani yetu katika dhabihu kuu ya Yesu, ambaye alimwaga damu yake kwa ajili yetu. (4) Tuna ushirika wa mmoja na mwingine. Tazama 1 Wakorintho 10:16-17**. Kikombe kile cha baraka tukibarikicho, je! Si ushirika wa damu ya Kristo? Mkate ule tuumegao, si ushirika wa mwili wa Kristo? Kwa kuwa mkate ni mmoja, sisi tulio wengi tu mwili mmoja; kwa maana**

**sisi sote twapokea sehemu ya ule mkate mmoja.** Neno komnyo linamaanisha ushirika. Katika muktadha, Paulo alisema kwamba kula katika Mahekalu ya sanamu huanzisha ushirika na mashetani. Vivyo hivyo, kula katika Meza ya Bwana tuna ushirika pamoja na Yesu na sisi kwa sisi. Tunatambua na kusisitiza umoja wetu kupitia utii wetu wenyewe kwa Kristo.

## Vitu vinavyotumika na Maana ya Meza ya Bwana

Maudhui ya Meza ya Bwana ni rahisi sana. Mtu hutaka kufanya kumbukumbu ya baadhi ya vitu vinavyodumu muda mrefu, kama vile matale, dhahabu, n.k. hata hivyo, Mungu alitengeneza kumbukumbu yake katika vitu viharibikavyo kama vile mkate na juisi ya dhabibu. Moyo wetu ndio utoao maana ya vitu hivyo. Yesu alitumia mkate usiotiwa chachu (Luka 22:1, 8-9). Wayahudi waliamriwa kutumia mkate usiochachwa katika sikukuu yao ya Pasaka, kwa hiyo Yesu alichukua kitu kinachofahamika na kukipa maana mpya. Sasa kinawakilisha mwili wa Yesu, ambao ulisulibiwa katika msalaba kwa ajili yetu. Yesu pia alichukua mzao wa mzabibu (Mathayo 26:29), ambayo ilikuwa ni juisi ya zabibu, na akasema kwamba sasa inawakilisha damu yake ambayo punde itamwagika juu msalabani.

Katika Mathayo 26, yesu alisema kuhusu mkate, **huu ni Mwili wangu** (26:26). Kuhusu mzao wa mzabibu alisema, **hii ni damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi**(26:28). Katika msingi wa maneno haya, baadhi ya watu wamekosea na kuhitimisha kwamba, pindi mkate na juisi

viinapobarikiwa hubadilika kihalisia na kuwa mwili na damu ya Yesu. Walichukulia kuwa ni sawa, ladha sawa, hali ya muonekano  ule ule kama awali, isipokuwa kwamba si vile vile. Hiyo si maana ya kifungu hiki. Yesu alimaanisha kuwa vinaashiria mwili wake na damu yake. Katika Yohana 10:9 Yesu alisema, "Mimi ndimi mlango." Yesu hakuwa akisema kuwa Yeye ni mlango halisi, ila kiroho alikuwa ni mlango wa mbinguni. Katika aya mbili baadaye, alisema kuwa Yeye alikuwa ni "Mchungaji mwema". Yeye ni mchungaji mkuu wa roho zetu (1 Petro 5:4). Yesu ni kama mlango au mchungaji. Kwa jinsi hiyo hiyo maudhui ya Meza ya Bwana yanatuashiria mwili na damu ya Yesu.

Katika 1 Wakorintho 11:24-25, Paulo aliwakumbusha Wakorintho maneno aliyoyatamka Yesu usiku ule alipoanzisha Meza ya Bwana na wanafunzi wake. Yesu aliwaambia wanafunzi wake,  **Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.** Tangu Yesu alipoanzisha Meza ya Bwana, ni muhimu. Si amri ya kawaida ya kanisa ambayo ilianzishwa miaka mingi baadaye na kanisa kuwasaidia Wakristo kukumbuka dhabihu ya Kristo. Ilitolewa na Kristo mwenyewe na imekuwa ikifanywa na Wakristo waaminifu tangu mwanzo wa kanisa. Tunaishiriki kwa kukumbuka dhabihu ya Kristo. Hata hivyo, hatupaswi kuichukulia kama ndio kipindi cha kuomboleza. Ni jambo la mkazo, kwa hakika. Pamoja na hayo, katika 1 Wakorintho 10:16, inaitwa "kikombe cha baraka." Katika baraka kuu tulizowahi kupokea.

## Lini tunashiriki Meza ya Bwana?

Kuna nyakati nyingi tofauti makanisa hushiriki Meza ya Bwana. Wengine wanaweza kufanya hivi mara moja kwa mwezi, mara moja ya robo ya mwaka au pekee katika matukio maalumu. Baadhi ya makinisa hushiriki kila juma. Mara nyingi watu watasema kuwa hakuna amri katika Biblia inayobainisha kuwa mara nyingi kiasi gani tushiriki. Ni kweli hakuna amri inayobainisha hasa ni mara nyingi kiasi gani tunapswa kushiriki. Lakini kama hakuna muda unaotarajiwa, hapo kama mtu akifanya mara moja katika maisha yake yote, yeye ni wa Maandiko kama mwingine ye yote.

Mfano wa kanisa la kwanza unaonesha kwamba sababu moja kuu ya kukutana ni kushiriki au "kumega mkate." Tunasoma Mdo 20:7, **na siku ya kwanza ya juma, tulipokuwa tumekutana ili kumega mkate, na Paulo akahutubu hadi usiku wa manane.** Hapa tunaona kwamba kanisa lilikutana ili kumega mkate, ambacho kilikuwa ni kipindi kingine cha kushiriki Meza Ya Bwana, na si tu kumsikiliza Paulo akihubiri. Pia tunajua kutoka maandiko ya kale ya Kikristo kwamba kanisa lilishiriki kila juma. Katika 1 Wakorintho 11:20 tunaona kwamba Wakorintho walikutana kwa lengo la kula Meza ya Bwana. Muda wa kukusanyika ulioamriwa ulikuwa ni siku ya kwanza ya juma (1 Wakorintho 16:2). Tunakutana kila siku ya kwanza, kwa hiyo tunapaswa kushiriki Meza ya Bwana kila siku ya kwanza ya juma.

Wengine huleta hoja kwamba kuifanya mara nyingi huondoa maana yake na kuifanya kama mila ambayo mtu huipitia. Kuna uwezekano huo, lakini jambo hilohilo lina ukweli pia katika matendo yote ya ibada, lakini hakuna hata mmoja anayehoji kuwa tunapaswa kufanya ibada kwa matukio maalumu tu. Paulo alizungumzia tatizo hili katika. 1 Wakorintho 11:28-29. **Lakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate, na kukinywea kikombe. Maana alaye na kunywa, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili.** Aya hizi mara nyingi zinaeleweka vibaya, na watu huamua kila wiki kama wanastahili au la, kwa kuzingatia jinsi wanavyojihisi kuwa wameishi maisha ya utakatifu kwa kiwango gani katika juma lililopita. Neno kutostahili ni kielezi ambacho hubadilisha namna ya chakula [meza ya Bwana] kinavyochukuliwa. Tunatakiwa kujihoji, hiyo ni, kuwa na uhakika kwamba tunakumbuka mwili wa Kristo na damu ambayo ilitolewa kwa ajili yetu. Hili ni jambo lenye uzito sana, kwa sababu Paulo alisema kwamba kama tutashiriki bila kufikiri juu ya hili, basi tunakunywa hukumu ya nafsi zetu. Hatujapoteza baraka tu, bali tumetenda dhambi!

## Nani anayepaswa kushiriki?

Wakati mwingine swali huulizwa, "Asiye Mkristo anaweza kushiriki Meza ya Bwana?" Ni lazima tukumbuke ya kwamba huu ni ushirika pamoja na Mungu na Yesu. Yesu anakula pamoja nasi katika ufalme. Ufalme ni kanisa, mwili wa kiroho wa Kristo, hivyo, hii ni baraka iliyohifadhiwa kwa washirika wa

ufalme wa Kristo tu. Baadhi ya ndugu wanataka kuweka mpaka nani anayeweza kushiriki, na wanagoma kuwaruhusu wale ambao wanawachukulia kuwa wako nje ya Kristo kushiriki. Tujiweke wenyewe katika jukumu la kuhukumu, na hatujaruhusiwa kuhukumu. Hatujui hali ya moyo wa mtu. Ni Meza ya Bwana, siyo meza yangu au meza ya kanisa. Ni ushirika. Kama mtu hayupo katika ushirika na Kristo, amepotea, na hakuna ushirika na Kristo. Yote anayofanya ni kula mkate mdogo na kunywa juisi tu. Roho yake haifaidiki au ubaya kuondoka kwa kuwa yeye tayari amepotea. Tunahitaji kuzingatia maisha yetu wenyewe pamoja na uhusiano wetu na Mungu na ufahamu wetu tunaposhiriki, na siyo kuwa hakimu wa wengine.

## Maswali ya kujipima

1. Taja mawazo manne makuu yanayohusiana na Meza ya Bwana.

2. Ni vitu gani viwili vinavyotumika katika Meza ya Bwana?

3. Akili zetu zinapaswa kulenga katika nini tunaposhiriki Meza ya Bwana?

4. Mifano gani miwili iliyotolewa kuonesha kwamba mkate na mzao wa mzabibu ni ishara tu?

5. Mara nyingi kiasi gani kanisa la kwanza lilishiriki Meza ya Bwana?

Kweli / Si kweli

1. Wakati mkate na juisi zinapobarikiwa, zinakuwa mwili na damu halisi ya Yesu. Kweli / Si kweli.

2. Yesu alichukua vitu vilivyo fahamika vya Siku kuu ya Pasaka ya Wayahudi na kuvipa maana mpya. Kweli / Si kweli

.

3. Kwa mtu kujihoji mwenyewe kunamaanisha kwamba aamue ni kwa kiwango gani amekuwa mtakatifu katika juma lililopita. Kweli / Si kweli.

4. Kwa kuwa Meza ya Bwana ni ya Wakristo pekee, viongozi wa kanisa wanatakiwa kulinda ili kuwa na uhakika kwamba ni Wakristo waaminifu ndio wanakula Meza ya Bwana. Kweli / Si kweli.

5. Kanisa lililoko Troa katika Acts 20:7 kimsingi walikutanika kumsikia Paulo akihubiri. Kweli / Si kweli.

# 5

## UIMBAJI

Matendo yote ya ibada yanapaswa kuwa ni ya kufurahisha kwa Mkristo, lakini kama kuna tendo moja ambalo linafurahisha zaidi kwa watu wengi, hilo litakuwa ni uimbaji. Mara nyingi watu huimba nyimbo zinazofahamika kwao wenyewe, kwa sauti ya juu au ya chini katika akili zao. Uimbaji ni sehemu muhimu katika ibada ya Mkristo, hata hivyo pia ni moja kati ya mambo yenye utata zaidi. Fungua akili yako na umwache Mungu azungumze nawe kupitia Biblia.

Aya mbili bora katika Agano Jipya zinazohusiana na uimbaji ni Waefeso 5:19 na Wakolosai 3:16-17**.** Zinafanana sana. **mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu;** (Waefeso 5:19). **Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu. Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye.** (Wakolosai 3:16-17).

## Kusudi la Uimbaji

Uimbaji ni njia ya kufundisha. Kwa maneno ya nyimbo tunazoimba, tunafundishana. Ni maneno tu yanayofundisha; kwa hiyo, ni lazima tuhakikishe kuwa maneno yanaeleweka vizuri, na ya kwamba yanafundisha somo la kiroho. Kuimba wimbo usiofaa ni sawa na kumfundisha mtu fundisho ovu. Siku zote tunaweza kukumbuka kanuni kwa urahisi kama tunaweza kuziweka katika muziki. Moja kati ya njia bora za kufundisha watoto ni kuwafundisha nyimbo. Wanaweza kujifunza kwa urahisi, na inafurahisha pia. Hivyo, uimbaji ni njia bora ya kufundishia. Wazo hili hata utengeneza sauti, ambapo ni maneno pekee ndiyo hufundisha na kujenga. Tunatakiwa kuimba nyimbo za rohoni, na si nyimbo ambazo tunazipenda au zinazosikika vizuri kwetu. Mara nyingi watu huuliza kuhusu utofauti baina ya zaburi, tenzi na nyimbo za rohoni. Ni vigumu kusema utofauti hasa. Maneno haya mara nyingi hutumika kwa mbadilishano, hivyo, inaonekana kwamba juhudi isichukuliwe katika kutofautisha aina tofauti za nyimbo.

Pia tunafundishana, ambapo huhimiza kitendo cha kujaliana katika ibada yetu. Matokeo ni kujengana kwa pamoja. Vitu vichache vinaweza kumtia mtu moyo zaidi kuliko nyimbo ambazo zinasisitiza umuhimu wa kanuni za Kiroho. Kwa kuwa tunatakiwa kufundishana, hii inahimiza kusanyiko lote lijihusishe katika kuimba, kuliko kuwa watu wachache pekee, kama vile kwaya au vikundi vidogo, ambapo wachache huimba na wengine husikiliza. Uimbaji ndicho kipengele pekee ambapo

kusanyiko zima linashiriki kwa sauti zinazofanana. Uimbaji dhabihu ya kiroho. **Basi, kwa njia yake yeye, na tumpe Mungu dhabihu ya sifa daima, yaani, tunda la midomo iliungamayo jina lake.** (Waebrania 13:15). Aya hii inarejea nyuma katika dhabihu za mfumo wa Agano la Kale na kutangaza kwamba uimbaji ni sehemu yetu ya kiroho kwa dhabihu za kimwili zilizotolewa katika Agano la Kale. Katika nyimbo zetu tunamtukuza Mungu kwa matendo yake makuu pamoja na kutoa shukurani kwa ajili ya zile baraka zake kuu. Hivyo, ni lazima tukumbuke tena kwamba tunawasiliana na Mungu katika uimbaji wetu. Uimbaji unahusisha utu wetu wote, roho, akili, moyo na midomo. Waefeso 5:19 inatuamrisha tuimbe kwa mioyo yetu. Tunapoimba, akili zetu na mioyo yetu ni lazima iwe pamoja na ujumbe wa wimbo, vinginevyo, uimbaji wetu si kitu ila ni ibada ya bure. Mungu hajawahi kupendezwa na ibada za bure.

Uimbaji huimiza umoja wa kanisa. Katika Warumi 15:6, Paulo akiwaomba Wakristo wa Kirumi wamtukuze Mungu kwa "akili moja na mdomo mmoja" Vifungu kadhaa vya Agano Jipya vinahimiza umoja wa kanisa, lakini uimbaji ni jambo moja la kuendeleza uhusiano wa karibu tunaopaswa kuwa nao sisi kwa sisi. Jambo la kuzingatia ni kwamba, ibada ya mtu kwa Mungu inaathirika pakubwa ikiwa umoja haupo miungoni mwa familia yetu ya kiroho. Vitu vichache vinainua zaidi inapotokea Wakristo walioungana kuimba pamoja nyimbo kama vile wanatokea katika mdomo mmoja.

## Jinsi Mungu Anavyoidhinisha!

Wengi hushindwa kuelewa jinsi tunavyopata mamlaka kwa ajili ya matendo yetu, hususani ibada yetu. Kuna aina mbili za amri, amri ya jumla na amri bainishi. Amri ya jumla ni maelezo ya ujumla yanayoidhinisha utendaji wa jambo bila ya kubainisha jinsi linavyotakiwa lifanyike. Kwa upande mwingine, amri bainishi hubainisha sawasawa namna jambo linavyopaswa kutendeka. Tazama baadhi ya mifano ya kawaida. Mungu anatuamuru twende tukahubiri injili, ambayo ni amri ya ujumla kwa sababu haikubainishwa ni njia gani itumike katika kwenda kuhubiri iliyotajwa. Nuhu aliambiwa atengeneze Safina ya mti wa mvinje. Aina ya mti ilikuwa ni amri bainishi, hivyo alikatazwa kutumia aina nyingine ya mti. Muziki ni neno la ujumla ambalo hujumuisha aina zote za muziki. Kama Mungu angesema tu fanyeni muziki, Wakristo wangekuwa na uchaguzi wa kutumia aina yo yote ya muziki lakini Mungu amebainisha uimbaji ambao unaondoa aina nyingine zote za muziki. Hivyo, ala za muziki zimeondolewa, ingawa Mungu hakutuambia wazi kuwa tusitumie ala.

## Historia ya Ala za Muziki

Vikundi vingi vya kidini vinatumia vyombo vya muziki kuambatanisha na uimbaji wao. Hili limekuwa la kawaida sana hata wachache huuliza kama ni sahihi. Hata hivyo, daima hiyo haijawa kesi. Ndani ya karne kadhaa tu zilizopita matumizi ya ala yamekua kwa kiasi kikubwa na hayaojiwi. Katika Agano Jipya tunaambiwa tuimbe pekee katika ibada, kwa kuwa ala za muziki

haijatajwa katika ibada. Kuna aina mbili za muziki, sauti (kuimba bila ala) na ala. Himizo katika ibada ni kuwa katika roho, ambapo msisitizo wa ala za muziki upo juu yetu au ni wa muda tu. Paulo aliamuru kafanya [hivyo], lakini alibainisha kwamba ala ilikuwa ni moyo. Wakolosai 3:17 inamwamuru mtu kufanya kila jambo katika jina la Yesu, hiyo ni, kwa mamlaka ya Yesu. Tunawezaje kuimba kwa mamlaka ya Yesu wakati tunaongeza ala ambazo hakuna mamlaka ya hilo? Maandiko yapo kimya kabisa kuhusu ala, hivyo wengi hudai kwamba kwa kuwa haikukatazwa, ni sahihi kabisa kutumia. Hata hivyo, ukimya hautengenezi mamlaka. Tunaona mifano miwili ya hili katika kitabu cha Waebrania. Katika Waebrania 1:4-5 mwandishi anatafuta kuanzisha ukuu wa Kristo dhidi ya malaika. Kufanya hivyo, anauliza ni kwa malaika gani Mungu alisema, “Wewe ni Mwanangu.” Kwa kweli, jibu ni hakuna. Kwa hiyo, Kristo ni mkuu kuliko malaika. Katika Waebrania 7:13-14 mwandishi akitafuta kuthibitisha ulazima wa ukuhani mpya ili Yesu aweze kuwa kuhani, sheria mpya ilipaswa kuja kwa sababu sheria ya kale haikusema kitu kuhusu kuhani kutoka katika kabila la Yuda. Badala yake, sheria ilibainisha kwamba makuhani wote wangekuja kutoka katika kabila la Lawi. Kwa kuwa Lawi imebainishwa, hiyo moja kwa moja inaondoa makabila mengine yote. Hivyo, Kristo hakuweza kuwa kuhani kulingana na sheria ya Musa, kwa sababu hakutokea kabila la Lawi. Vivyo hivyo, kwa kuwa uimbaji umeidhinishwa, aina nyingine zote za muziki zimeondolewa. Kwa maneno mengine, hatuna mamlaka ya kutumia vyombo vya muziki katika ibada. Historia nzima ya Ukristo, ala za muziki zimekuwa

zikipingwa mara kwa mara. Mababa wa kanisa mara kwa mara waligoma ongezeko la ala [za muziki] katika ibada zao. Kwa karne nyingi hakuna kanisa lililotumia ala za muziki. Chombo cha kwanza inaamika kuanza kutambulishwa mwishoni mwa karne ya saba. Wayahudi walitumia ala katika ibada zao za hekaluni, na Wayunani walitumia katika ibada zao za sanamu. Kwa hiyo, Wakristo wa mwanzoni bilashaka wengi walifahamu na wangejisikia vizuri na ala (kutumia), pamoja na hayo inasadikika kwa vitendo na kila mmoja kwamba kanisa la kwanza halikutumia ala [za muziki] katika ibada zao za kidini. Nyongeza, waanzilishi wengi wa madhehebu ya kisasa pia walipinga matumizi ya vyombo vya muziki. Zingatia nukuu hizi chache:

- Martin Luther: "Chombo [cha muziki] katika ibada ya Mungu ni bendera ya Baal."

- John Calvin: " Si sahihi tena kuliko kuchoma uvumba, mwangaza wa tambi, au uamsho wa vivuli vingine vya sheria. Wakatoliki wa Kirumi walikopa kutoka kwa Wayahudi."

- John Wesley: "Sina pingamizi kwa chombo katika ibada zetu ikiwa hakionekani wala kusikika."

- John Knox aliita chombo "kifua cha filimbi."

Lengo letu ni kulirejesha kanisa la Agano Jipya, ambalo kamwe halikutumia na kupinga vikali matumizi ya ala za muziki katika ibada. Kwa hiyo, kama mtu anatafuta kuwa Mkristo wa Agano Jipya, ataabudu bila ya ala.

## Maswali ya kujipima

1. Lengo kuu la uimbaji ni lipi?

2. Uimbaji ni dhabihu ya______________________.

3. Aina mbili za amri ni zipi?

4. Tumeamriwa kuimba kwa ______________ yetu.

5. Kwa nini ilikuwa haiwezekani kwa Kristo kuwa kuhani kulingana na Sheria ya Musa?

Kweli / Si kweli

1. Kuna tofauti ndogo baina ya zaburi, tenzi, au nyimbo za rohoni. Kweli / Si kweli.

2. Sehemu ya muhimu zaidi ya wimbo ni mvuto na kusisimua. Kweli / Si kweli.

3. Kutoka mwanzoni kabisa mwa kanisa, matumizi ya ala katika ibada yamekuwa yakijadiliwa kwa kiwango cha juu. Kweli / Si kweli.

4. Kwa kuwa Biblia haijatuzuia kutotumia ala, tunajua Mungu anapendezwa na matumizi yake. Kweli / Si kweli

.

5. Waanzilishi wa madhehebu mengi ya kisasa pia walipinga matumizi ya ala. Kweli / Si kweli.

# 6

## MAKUSANYO YA WATAKATIFU (MATOLEO)

Matoleo au makusanyo ni baraka muhimu kama ulivyo wajibu wa Mkristo. Bila shaka kielelezo kikuu cha kutoa ni Yesu kufa msalabani kwa ajili yetu. Katika Marko 12:41-44 tunaona uwezekano wa kielelezo kikuu ambacho mwanadamu anaweza kutoa. Yesu alikuwa akiwaangalia watu wakitia fedha katika sanduku la hazina hekaluni. Mjane mmoja fukara akaja na kuweka senti mbili za fedha, ambazo zilikuwa ni sarafu ndogo katika mzunguko kwa wakati huo. Bila shaka, kiasi kile kwa kiwango cha fedha za leo kingekuwa ni tofauti, lakini wacha niseme kwamba kisingekuwa na thamani kubwa. Bado Yesu alisema kuwa huyu mjane fukara ametia fora kuliko wao wote, kwasababu walitoa ziada ya mali zao, wakati yeye alitoa vyote alivyokuwa navyo.

### Dhamira ya Kutoa

Dhamira siku zote ni muhimu kwa Mungu. Kwanza, tuangalie baadhi ya dhamiri mbaya kwa matoleo. Hatupaswi kutoa tu kwa dhana ya wajibu, shahuku kwa ajili ya heshima au kutukuzwa na watu, au kuzipa fahamu zetu unafuu kwa ukosefu wa kutohusika. Kutoa kiasi fulani cha pesa hakutapunguza hitaji la mtu kufanya kitu fulani binafsi. Hakuna mtu awezaye kumuajiri mtu mwingine amtumikie Mungu kwa ajili

yake. Kimsingi kutoa ni tendo la imani, upendo na ibada kwa Mungu kwa upande wa mkristo. Kwa kutoa tunathibitisha upendo wetu kwa Mungu. Tunapotoa, tunakua pia. Tunakua washirika wa asili ya Uungu kwa kuwa wakarimu. Kutoa pia kunafungua mlango kwa Mungu kutubariki. Mwisho, tunatoa kwa ajili ya kanisa, ufalme wa Mungu ukue. Fedha inahitajika kwa mahitaji mbalimbali ya kanisa, na ni mpango wa Mungu kwa watoto wake kuutegemeza ufalme. 1 Wakorintho 16:1-2 **Kwa habari ya ile changizo kwa ajili ya watakatifu, kama vile nilivyoamuru makanisa ya Galatia, nanyi fanyeni vivyo. Siku ya kwanza ya juma kila mtu kwenu na aweke akiba kwake, kwa kadiri ya kufanikiwa kwake; ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja;** katika aya hizi tunaona amri ya kutoa au kuweka akiba. Kwa kuwa tumeamriwa kufanya hivyo katika siku ya kwanza ya juma wakati ambao kanisa ukutanika, hii inaashiria kuweka akiba ilikuwa ni changizo llilotolewa kwa kanisa na si kuweka nyumbani. Kama kuweka akiba lingekuwa ni jambo ambalo mtu anaweka nyumbani, basi hilo lingeweza kufanywa muda wowote na si mpaka mtu asubiri kukusanyika kanisani.

- Hii ilikuwa ni amri binafsi. Kila mmoja anapaswa kushiriki, na si tajiri pekee, mzee, , wale wenye deni kidogo, n.k.

- Tunatakiwa kuweka akiba. Mara nyingi tunadhani changizo kuwa ni pesa tu, lakini pia inaweza kuhusisha vitu vingine, kutegemea na kile mtu anachoweza kuwa nacho. Eti kwa sababu mtu ana fedha

kidogo haimaanishi kuwa hawezi kutoa. Biblia kamwe haijabainisha kuwa ni pesa tu ndiyo inayoweza kutolewa.

- Tunatakiwa kutoa kwa kadiri ya kufanikiwa kwetu. Mungu hajabainisha ni kiwango gani tunalazimika kutoa. Wayahudi waliamriwa kutoa fungu la kumi, lakini kuzingatia dhabihu mbalimbali na vitu vingine kwa hakika walitoa zaidi ya hivyo. Je, kwa sheria bora na Mwokozi bora, tunapaswa kutoa kidogo? Jambo la msingi hapa ni kwamba hatuwezi kujilinganisha na wengine. Kutoa ni suala la mtu mmoja mmoja, hivyo tunapaswa kuepuka kujaribu kujitetea kwa kulinganisha matoleo yetu na wengine ambao wanaweza kutoa kidogo sana.

- Hiki kilikuwa kizuizi. Walitakiwa kukusanya changizo ili kwamba kusiwe na mchango pindi Paulo atakapokuja. Hii ilikuwa ni juu ya ujio wa haraka wa Paulo huko Korintho. Walitakiwa kuwa na mchango wao tayari kwa ajili ya Paulo atakapowasiri. Hii inatuonesha kwamba tunatakiwa kuwa na fedha tayari kwa ajili ya mahitaji ambayo yataibuka na sio siku zote kusubiria hitaji lijitokeze ndipo tukusanye mchango.

2 Wakorintho 9:5-7
**Basi naliona ya kuwa ni lazima niwaonye ndugu hawa watangulie kufika kwenu, na kutengeneza mapema karama yenu mliyoahidi tangu zamani, ili iwe tayari, na hivi iwe kama kipawa, wala si kama kitu kitolewacho kwa unyimivu. Lakini nasema neno hili, Apandaye haba atavuna haba; apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu. Kila mtu na atende kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa huzuni, wala si kwa lazima; maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu.**

- Tunatakiwa kutoa kwa moyo wa ukunjufu na kwa hiari. Mungu hapendezwi kama tukitoa kwa sababu tu tunajihisi kama inatubidi tutoe. Tunatoa kwa roho ya upendo na si kwa lazima. Kutoa kamwe hakupaswi kuchukuliwa kuwa ni kitu kigumu au ni kazi ngumu. Baadhi ya makanisa wanajaribu kuwalazimisha washirika wao kutoa kwa kuweka ahadi na kisha kutuma ujumbe wa madai kama hawawezi kutoa yote waliyoahidi. Hii inaondoa ukunjufu katika utoaji, hivyo kulifanya kuwa ni jambo gumu.

- Tunatakiwa kutoa kama tulivyokusudia mioyoni mwetu. Hii inamaanisha kwamba tunafanya maamuzi tukiwa na ufahamu na akili kabla juu ya kile cha kutoa. Kwanza tunafanya maamuzi nini cha kumpa Mungu halafu vinavyobaki tunatumia, sio siku ya Jumapili tunatoa masalia.

- Kifungu hiki pia kinatuhamasisha kutoa. Sababu moja kubwa kwa nini kutoa hakupaswi kuchukuliwa kuwa ni jambo gumu ni kwa sababu Mungu ametuahidi kutubariki zaidi kuliko hata tutoavyo. Hatupaswi kutoa kwasababu ya tamaa, hiyo ni, kwa shahuku ya kupata zaidi; pamoja na hayo, Mungu ameahidi kutubariki tunapotoa. Wengine, hususani wainjilisti wa runinga, hutumia vibaya kifungu hiki kwa kuchochea tamaa ya mtu kupokea zaidi. Wanaweza kumtia mtu moyo awatumie “mbegu ya fedha” na hivyo, haraka sana mtu huyo atapokea hitaji lake. Hii huleta dhamira mbaya na pia si jambo la kimaandiko. 2 Kor 9:8 inatuambia kwamba Mungu atatubariki ili kwamba tuweze kuitumia kwa ajili ya kazi nyingine njema, sio kutumia tu kwa mambo yetu wenyewe na anasa.

- Kiwango cha zawadi si muhimu. **Maana, kama nia ipo, hukubaliwa kwa kadiri ya alivyo navyo mtu, si kwa kadiri ya asivyo navyo.** (2 Wakorintho 8:12). Kwa maneno mengine, Mungu haangalii tu kiwango cha zawadi ya mtu. Hii inaelezea kwanini hatuwezi kulinganisha zawadi zetu. Mungu ana hukumu kulingana na uwezo wa mtu, na Mungu pekee ndiye awezaye kuamua hilo kwa ukweli.

## Matokeo ya Utoaji

Matokeo mojawapo ya wazi ya utoaji ni kwamba mahitaji ya kanisa yanajazwa [kutatuliwa]. Hatupati mamlaka yoyote katika Biblia kuwa na miradi mbalimbali ya kupata fedha au kujihusisha na biashara ili kupata fedha na kuwezesha shuguli mbalimbali za kanisa, wala kanisa halipaswi kujiingiza katika kuomba michango kwa wasio washirika [wasio Wakristo], kama ilivyo kawaida katika vipindi vingi vya runinga leo. Kazi ya kanisa inapaswa kubebwa na washirika wake. Kutoa huzaa shukurani na utukufu kwa Mungu. Kwa kuhitimisha huduma yetu kwa Mungu, wengine wengi huona uthibitisho wa huduma yetu na kumtukuza Mungu kwa njia ya utiifu wetu wa amri ya Mungu. Tunamuona Kristo akizungumza kuhusu hili katika Mathayo 5:16, **Nuru yenu na iangaze kwa watu, ili kwamba wayaonapo matendo yenu mema wapate kumtukuza Baba yenu wa mbinguni.** Katika utoaji, kanisa na sisi tunakuwa kiroho. Tunapotoa tuwezavyo, kanisa linakuwa na mifuko ya kufanya kazi yake, ambayo itapelekea katika kuongoa roho zilizopotea katika maeneo mengi. Wachache ndio hutaka kuwa sehemu ya kanisa ambalo hakuna kinachoendelea. Watu wanapoona kanisa likifanya kazi, Mungu anatukuzwa, na watu watataka kuwa sehemu ya kanisa pale ambapo mambo mazuri hutokea [kufanyika].

## Maswali ya kujipima

1. Kiasi gani cha pesa mjane fukara alitoa hekaluni kwenye sanduku la hazina?

2. Kiasi gani Wayahudi waliamriwa kumtolea Mungu?

3. Maana yake nini mtu atoe kama alivyokusudia moyoni mwake?

4. Mungu anampenda yeye ________________ ukunjufu.

5. Kutoa huzaa ______________na _______________ kwa Mungu.

Kweli / Si kweli

1. Kutoa kwa ukarimu ni njia nzuri ya mtu kuongeza utajiri kwa sababu Yesu aliahidi kuwabariki wale watoao kwa ukarimu. Kweli / Si kweli.

2. Ni wale pekee wenye pesa za “ziada” ndio wanaopaswa kutoa kuwezesha kazi ya kanisa. Kweli / Si kweli.

3. Kimsingi kutoa ni tendo la imani, upendo na ibada kwa Mungu. Kweli / Si kweli.

4. Haijalishi sana kwanini tunatoa, maadam tunatoa kwa muda mrefu. Kweli / Si kweli.

5. Kiwango cha zawadi zetu ni sababu kubwa katika kujua kama zawadi yetu imekubaliwa na Mungu. Kweli / Si kweli.